**Learning by Ear 2010**

**Theme: Illiteracy and education**

**“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 08:** *“Kipendacho moyo…”*

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor:** Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas

**Characters:** **Elinam** *(ana umri wa miaka 22 , mtoto wao Papa Wali na Mamoua, na ni kaka yake Latifa. Amehitimu hivi karibuni kwa shahada ya uzamili kwenye somo la uhandisi. Bado hajaajiriwa na angali anaishi jijini alikosomea chuokikuu ambako ni kilomita kiasi 120 kutoka katika mji mdogo wanakoishi wazazi wake. Amekuwa kwa muda mrefu akiugua kisiri kwa mapenzi yake kwa Zakia)*

**Zakia** *(Mwanamke mwenye umri wa miaka 23, ni mwanamke mwenye uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki wa dhati wa Latifa na amepandishwa cheo kuwa mkurugenzi wa utangazaji wa shirika lake la Safari za Kitalii na angali akifanya kazi katika mji mdogo ambao yeye na Latifa wanatoka.)*

**Latifa** *(Ana umri wa miaka 18, ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Anafanya mazoezi katika zahanati ya maradhi ya macho baada ya kuhitimu kuwa daktari msaidizi. Amekuwa akiishi na kaka yake jijini kwa miaka zaidi ya mitatu)*

**INTRO**

**Hujambo msikilizaji na karibu kwenye sehemu ya nane ya kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako: mfululizo wetu wa makala ya "Mtoto wa kike ahitimu shuleni" kuhusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Tangu alipomtia machoni Zakia kwenye maonyesho ya utalii, Elinam ametumia fedha zake nyingi kuwasiliana naye kwa simu. Wanazungumzia mengi ila Elinam mpaka sasa hajamuarifu kuhusu hisia alizonazo kwake.*
*Dada yake Latifa, naye amegeuka kuwa mchache wa maneno. Kila mara anaonekana kama ana mawazo mengi. Anajaribu juu chini kufaulu kwenye mazoezi yake ya muda wa miezi sita anayofanya kwenye zanahati ya macho. Alianza mazoezi hayo baada ya kuhitimu kuwa daktari msaidizi.*
*Wakati huo huo,akili yote ya Zakia i kazini kwake kwenye shirika la maswala ya utalii. Elinam si chochote si lolote ukimlinganisha na wanaume wengine ambao ni vijana na matajiri anaokutana nao Zakia kazini mwake.*
*Hata hivyo, leo Elinam ameupiga moyo wake konde na atamueleza Zakia yalo moyoni hata ikiwa ombi lake litakataliwa.Hii ni sehemu ya nane:* ***Kipendacho moyo…Sikiliza!***

**Scene 1, IN ZAKIA'S OFFICE**

Zakia na Elinam on the phone

1. **SFX ATMO: OFFICE SOUNDS – UNCLEAR VOICES – PHONE RINGING – PRINTER**
2. **SFX ATMO: LANDLINE RINGING**

3. **Zakia:** Naam, hallo?

4. **Elinam:** Vipi, Zakia !

5. **Zakia:** Poa, Elinam! Habari gani?

6. **Elinam:** Nzuri sana nashukuru! Na wewe je?

7. **Zakia:** Sijambo, ila najihisi mchovu kidogo. Cha mno?

8. **Elinam:** Aaah…Eeem… Nilitaka tu kusikia sauti yako...

9. **Zakia:** Alaa, kweli? (**laughing**) Nadhani si mbaya sana!

10. **Elinam:** (**Softly**) Ni kama ya malaika!

11. **Zakia:** Hujawahi kunitaka nikutendee hisani, basi mbona unanitania?

12. **Elinam:** Sikutanii! Ninayosema ni ukweli. (**Emphasising**) Sauti yako inanivuruga, inanizuga na kupeleka hisia zangu mahala pasipoelezeka!

13. **Zakia:** (**Amused**) Kwani ulisoma somo lisilokufaa katika chuo kikuu? Afadhali ungesoma masomo yanayohusiana na sanaa, hususan mashairi! Ama unaniona mimi kuwa mahali rahisi unapoweza kuvukia mto?

14. **Elinam:** La hasha, sivyo unavyofikiria. Kusema kweli wewe ni tunu au niseme kito cha thamani.

15. **Zakia:** Iweje ghafula bin vuu nina hizo sifa unazonisifia. Kwani umepiga simu namba ambayo hukuikusudia?

16.**Elinam:** Kwa kuwa sijakuarifu hayo haina maana kwamba sijawahi kuyawazia.

17.**Zakia:** Alaa! Fundi huyo hapo bingwa wa kila jambo!

18.**Elinam:** Ninahitaji ubingwa au ufundi gani kukueleza kwamba nimerowa kwa mapenzi yako?

19.**Zakia:** (**Silence**) …

20.**Elinam:** Upo?

21.**Zakia:** (**Very reserved**) Naam, Nakusikiliza…

22.**Elinam:** Umeshayapata hayo ambayo nimekuarifu?

23.**Zakia:** Tafadhali unaweza kuikata simu nami nitakupigia kwa simu yangu ya mkono?

24.**Elinam:** Sawa, tutazungumza baadaye.

25.**SFX ATMO: SOUND OF STEPS PACING UP AND DOWN**

26.**Zakia:** (**Loud sigh**) Mungu wangu!

27.**SFX ATMO NUMBER BEING DIALED ON A MOBILE**

28.**Elinam:** Hallo?

29.**Zakia:** Naam! Nakusikiliza wewe…

30.**Elinam:** Nimekuuliza swali...

31.**Zakia:** Nikumbushe?

32.**Elinam:** Unadhani ni nadharia kuwa nakupenda?

33.**Zakia:** Unajua vizuri kuwa leo si siku ya wajinga, sivyo?

34.**Elinam:** Kuna siku kweli utaniamini nikikwambia jambo la kweli?

35.**Zakia:** Siku ambayo utakoma kunichezea akili yangu!

36.**Elinam**: Kusema la haki ninalolisema ninalisema kwa dhati ya moyo wangu!

37.**Zakia**: Naona kama unafanya mchezo!

38.**Elinam**: Ina maana kuwa ombi langu limekataliwa?

39.**Zakia**: Sijui niseme nini.

40.**Elinam**: Nambie endapo tunaweza kuwa na uhusiano mimi na wewe

41.**Zakia**: (**A little annoyed**) Nimekuwa rafiki ya mdogo wako kwa miaka takriban kumi. Hukujishughulisha nami tulipokuwa shuleni. Hata kwenye maonyesho hukuzungumza nami sana. Mara moja hii umezuka ukinieleza hayo kisha unataraji nikukimbilie nikukumbatie. Ni kwa kuwa sasa umeshahitimu kuwa mhandisi au vipi?

42.**Elinam**: Samahani sana! Haikuwa nia yangu kukuudhi. Kwamba nimeshahitimu kuwa mhandisi siyo sababu ya mimi kusema haya. Nilichelea kukueleza hisia zangu kwako. Nilitahayari. Lakini sasa nimekiri kwamba moyo wangu umekuchagua na inanibidi nikueleze!

43.**Zakia**: (**Mockingly**) Ndugu yetu amezitupilia mbali haya zake na sasa anataka uhusiano wa kimapenzi na dadake.Unajua kwamba mimi nimekuzidi umri kwa mwaka mmoja?

44.**Elinam**: Umri si hoja. Inategemea na msimamo wa mtu.

45.**Zakia**: (**Mockingly**) Tangu lini msimamo wako ukaelekea huko unakoelekea?

46.**Elinam**: Kwa hisani yako Zakia, niamini ninayokuambia! Nimejitahidi kukabiliana na hisia zangu kuweka bayana hisia zangu. Ninakuheshimu sana... desturi zako, elimu yako, ujasiri wako, na kila jambo ulilomfanyia mdogo wangu, maadili yako... Ninajua kuwa mimi si wa tabaka lako, nalielewa hilo...

47.**Zakia**: (**Sighing, a bit disoriented**) Tafadhali, Elinam, mbona tusiyazungumzie mambo haya baadaye? Sijui niseme nini... na ningali afisini... jambo hilo limenizukia ghafla....kisa chote...

48.**Elinam**: Si kisa, Zakia, hatimaye nimepata kukuelezea hisia zangu.

49.**Zakia**: (**Silence**)

50.**Elinam**: Upo?

51.**Zakia**: (**Sighing**) Nitakupigia simu usiku, sawa?

52.**Elinam**: Sawa… Asante kwa kunisikiza. Nakutakia kila la heri!

53.**Zakia**: Asante! Kwaheri!

**MUSIC**

54.**NARRATOR**: *Baadaye usiku, Elinam yuko chumbani kwake akisubiri kwa hamu simu ya Zakia. Anasikia sauti ambayo hakuielewa iliyotokea chumbani kwa mdogo wake. Anakwenda kuchunguza kinachomsumbua Latifa ambaye hajakuwa akimtia shughuli katika muda mfupi uliopita..*

## Scene 2, IN LATIFA'S ROOM

Elinam na Latifa

55.**SFX ATMO: NOISE OF BED SPRINGS, APPROACHING FOOTSTEPS IN ROOM (ELINAM), DOOR BEING OPENED AND SHUT**

56.**Elinam**: Latifa, kuna nini?

57.**Latifa**: (**Sniffling**)

58.**Elinam**: **(softly)** Latifa, kuna shida gani?

59.**Latifa**: (**Sniffling**) Hakuna kitu…

60.**Elinam**: Haiwezekani kuwa unalia bila sababu?

61.**Latifa**: (…)

62.**Elinam**: Kwani nimekukosea?

63.**Latifa**: Hapana…

64.**Elinam**: Kwani kuna matatizo kazini?

65.**Latifa**: La hasha…

66.**Elinam**: Una matatizo ya kifedha?

67.**Latifa**: (**Silence**) Wala sina…

68.**Elinam**: Bila shaka, una sababu inayokuliza.

69.**Latifa**: (**Silence**)

70.**Elinam**: Unatamani kwenda nyumbani?

71.**Latifa**: (**Silence**)

72.**Elinam**: (**Coaxing her**) Ninajua sijawa nikikushughulikia. Wajua, hali yangu ngumu kwa kuwa sina kazi hata baada ya miaka mingi ya kujibidiisha na kujihini kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo wewe ungali mdogo wangu mpendwa na ningependa tuelezane kila jambo linalotufika. Kwa hivyo kwa hisani yako niambie kinachokuliza.

73.**Latifa**: (**Wiping her tears and blowing her nose**) Daktari mkuu wa zahanati yetu leo ameniambia kwamba nilipoteza wakati wangu bure nilipokiacha cheti cha kumaliza shule ya sekondari na kutosomea udaktari katika chuo kikuu.. Aliniiambia ningekuwa na kazi nzuri!

74.**Elinam**: Kwa hivyo unanilaumu mimi kwa kukupendekezea uwe daktari msaidizi?

75.**Latifa**: Hapana… Sikulaumu…

76.**Elinam**: (**Silence**) Wajua, sikutaka ukose kabisa nafasi ya kusoma.

77.**Latifa**: Usijitetee, si kosa lako. Mama na Baba hawakunipa moyo, vinginevyo leo ningekuwa nikisoma katika chuo kikuu!

78.**Elinam**: Latifa, usijitie dhiki kwa jambo hili, vinginevyo utazidi kusumbuka maishani hata kama utafanikiwa kwa kiasi gani. Ninaona fahari kwamba umepata elimu lakini ninakereka nikiona jinsi unavyojitesa kwa fikra kiasi cha kumsemesha vibaya yeyote anayekuzungumzia.

79.**Latifa**: (**Still crying)** Sikulaumu hata kidogo.

80.**Elinam**: Hapana, lakini unadhani ninahisi vipi ninapokuona ukilia? Nilikusaidia ili uyaepuke maisha duni ya kuwa mamawa nyumbani huko vijijini. Tumejitahidi kwa muda mrefu ili leo kusiwe na machozi. Tungefanya kipi zaidi ya tulichofanikiwa ukilizingatia pato letu dogo? Unajitatiza bure. Mara kwa mara unaonekana mwenye huzuni... Jitizame jinsi ulivyo. Mtoto wa umri wa miaka 19 hapo ulipo lakini mtu akikutazama atafikiri una umri wa zaidi ya miaka thelathini!

81.**Latifa**: Hali ya baba imeimarika lakini hajatusaidia kwa vyovyote. Kwa nini nisilie?

82.**Elinam**: Niliukatiza uhusiano na wazazi wetu kitambo kwa kuwa hawaelewi mambo. Hata hivyo tunapaswa kuwasamehe hata tunapokabiliwa na hali ngumu. Mama na Baba wanasumbuliwa na kutojua kusoma na kuandika. Unawataraji waelewe na wapende kitu ambacho hawakijui? Inatubidi kubadilisha hali ya mambo ili tuibadili hali ya kizazi kijacho.

83.**Latifa**: Lakini bila cheti changu cha shule ya upili, nina tofauti gani na mtu ambaye hajasoma?

84.**Elinam**: Nadhani unafanya mzaha,ama sivyo!**Laughter**) Lau ungekuwa kweli hujasoma hungekuwa ukilia. Unalia kwa kuwa umegundua umuhimu wa elimu.

85.**Latifa**: Ninalia kwa sababu naona wigo wangu si mpana kwavile mimi ni daktari msaidizi tu.

86.**Elinam**: (**Getting angry**) Shukuru Mungu kwa kuwa unavaa sare nyeupe na unalipwa marupurupu unapofanya mazoezi yako. Sina chochote ingawa nina shahada ya uzamili. Sina hata mahala ninapofanya mazoezi bila malipo, usiyaanze… Endelea kulia kama unaona litakusaidia! (**He gets up and opens the door**)

87.**SFX: FOOTSTEPS (ELINAM) GOING AWAY. DOOR OPENING.**
88.**SFX: DOOR SLAMMING**
89.**SFX: DOOR OPENING**

90.**Elinam**: Kabla sijasahau! Napanga kuenda nyumbani mwishoni mwa juma hili kuona jinsi tunavyoweza kumsaidia mdogo wetu!

91.**Latifa**: (**Sulking**) Naam, Sawa! Sema unakwenda kukutana na Zakia!

92.**Elinam**: Haya ya Zakia yametokea wapi?

93.**Latifa**: Ahaa, unaniona mpumbavu, siyo?

94.**Elinam**: Hebu nambie unayoyajua?

95.**Latifa**: (**Sarcastically**) Bwana, hayo ni yako, si yangu! Uwe na safari njema! Na mwambie nimeshakizoea kimya chake. Ameshapata mwengine wa kuwasiliana naye hata hivyo!

96.**Elinam**: (**Smiling**) Wewe, una mambo mtoto wa watu!

97.**Latifa**: Sina haja ya kushughulisha akili yangu na visa vya mapenzi ya watu!

98.**Elinam**: Unanichokoza? Kuna jambo wataka kujua?

99.**Latifa**: Nitake nini? Nikitaka kukutana nawe, nitamjulisha Zakia akuzuie!

100. **Elinam**: Huo ni wivu ninavyohisi!

101. **Latifa**: Nani awe na wivu? Mimi? (**Laughing like a gossip**)

102. **Elinam**: Jitafutie mpenzi! Hapo utakuwa na wakati mzuri.

103. **Latifa**: Nakutakia safari njema! Bwana mapenzi!

**MUSIC**

**OUTRO**

*Suala la mapenzi limejitoma maishani mwa watoto wa Papa Wali na Mamoua. Moyo wa Elinam umerowa kwa mapenzi huku Latifa akimwonea wivu. Ingawa maneno ya Elinam ni muhimu, inaelekea Zakia amesahau ahadi yake kumpigia simu. Elinam alisubiri hadi akatwaliwa na usingizi. Je Elinam atakwenda nyumbani kama alivyoahidi?Kipi kinachomsubiri nyumbani kwa wazazi wake? Je Zakia atamkubali? Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu itakayofuata ya "***Mtoto wa kike ahitimu shuleni***", mfululizo unaohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.*

**Ukitaka kukisikiliza kipindi hiki tena au vipindi vyengine vya Noa Bongo-Jenga Maisha yako , tazama ukurasa wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe. Anwani ni :** lbe@dw-world.de

**Tumefika tamati kwa leo.Hadi wakati mwengine kwaheri!**

**END OF 8th EPISODE**